**R745**

## BUSARA KAMA NYOKA NA WAPOLE KAMA NJIWA

“Angalieni, mimi nawatuma kama Kondoo kati ya mbwa mwitu, basi iweni na busara kama nyoka na kawa watu wapole kama njiwa” **Mathayo 10:16**

Bwana wetu alisema hivi alipowatuma mitume wake mara ya kwanza kutangaza injil. Walikuwa wanaenda kuokoa wanadamu kutokana na mauti. Oparesheni hiyo ingekuwa mwiongoni mwa matabaka na sampuli ya watu mbali mbali. Wao wenyewe wangekumbana na mateso hata na kifo. Wange kutana na kukataliwa na upinzani mkali. Hali ya kutoamini na ugumu wa moyo unge wazuia katika kila hatua. Walikuwa na mwito muhimu sana kutekeleza. Ilikuwa muhimu sana hivi kwamba iliwabidi kutimiza lengo lao. Kristo aliwapa muongozo huu kwa jumla kuwa kigezo cha matendo yao, ili kuwaongo wanapotekeleza wajibu wao. Asili ya mwanadamu hufanana katika enzi zote, na mpango wa Mungu ni ule ule. Na bila shaka, mwongozo leo hii ni mzuri tu jinsi ulivyokuwa miaka mia nane zilizopita.

Kwa nini Mwokozi wetu achukue nyoka kama mfano wa busara kwao kuiga? Lazima kuwe na sababu. Hataki wale wanaokwenda kushika nafsi kuiga nyoka isipokuwa katika suala la hekima yake. Ndiposa kwa hali hiyo anafanya. Tabia za nyoka ni za kipekee, na zina somo la mafundisho. Mbona Bwana asiwaambie watumishi wake wawe na busara kama simba, mbwa mwitu, au wanyama wengine wakali? Kwa nini uchague nyoka?

Yeyote ambaye amekwishaipa jambo hilo tafakari yoyote anaweza kujibu kwa urahisi. Nyoka, katika kumkaribia mawindo yake, hamkimbilii kwa njia ya kumshtua, kumdhalilisha, na kumtorosha, kama vile wanyama wengine hao ufanya. Njia zake ni za tahadhari sana, na bado zinafaa. Yeye hutembea kwa njia ya uangalifu zaidi iwezekanavyo, asijekutahadharisha pasi na haja, na anajidhihirisha kwa njia ya kumvutia yule ambaye anatafuta kumfikia. Iwapo ni lazima, asubiri kwa muda mrefu na kwa uvumilivu, mawindo yake anapokimbia au kuruka huku na kule, bado atabakia katika nafasi hiyo ambayo itamfaa zaidi. Kwa hivyo, mawindo, akiwa amevutwa kwake, hujileta karibu, na hapo ananaswa. Nyoka anapoinuka ili kupata mawindo yake, ni mara chache anakosa kufaulu kutimiza lengo lake. Katika haya yote inaonekana hekima ya pekee ya kiumbe hichi. Paka au mnyama yeyote mharibifu anapomngojea mawindo yake, kawaida hujificha mpaka amrukie; tendo ambalo humtahadharisha mawindo yake. Lakini nyoka mara nyingi hujidhihirisha kikamilifu apate kuonekana, na kwa mavutio ambavyo anawasilisha, anamnasa mawindo yake.

Mwokozi wetu anawaagiza wafuasi wake kuiga busara ya nyoka, huku wakiwa wapole kama njiwa. Hawashiki nafsi za kuharibu, bali kuokoa. Ikiwa wanataka kutimiza jambo hili nzuri, wanapaswa kutumia busara. Wajibu ndiyo inafaa zaidi na bora kabisa kiwezacho kuvutia umakinifu wa watu. Kwa hivyo hekima ya hali ya juu inapaswa kutumika kuikamilisha.

Akili ya binadamu ni ngumu sana kudhibiti. Hivyo ni muhimu jinsi gani kwamba wote ambao wanawasilisha ukweli wa Mungu kwayo, aidha kama wahudumu, wasambazaji wa nakala, au kwa mazungumzo ya kawaida lazima waelewe jukumu lao. Ni rahisi sana kupitia mazungumuzo, ya dakika kumi tu kuwacha maoni ya kudumu akilini ambayo hayawezi kuwa rahisi kufutika.

Madhara mengi sana yamefanyiwa jitihada za ukweli katika siku zilizopita, na watu katika jamii, watu waliokuwa na wepesi wa "kuingia tu," jinsi inavyosemekana , na kuanzisha mjadala na mabishano, kwenye kona za barabara au kwenye maduka, au mahali popote palipokuwa na nafasi ya kujazana, juu ya

ukweli, hata kama watu hawataki, mpaka watu watakapochukizwa, na kwa njia hiyo masikio yao hayawezi kufikiwa tena. Huu sio busara ya nyoka. Haufanani nayo.

Hao hawafuati mwongozo wa Petero. Wanaweza nukuu sehemu tu ya maagizo yake, lakini wanasahau au kupuuza mengine.. "Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu, awaulizaye sababu ya tumainai lililo ndani yenu, kwa upole na kwa hofu. Bali ni nadra sana kwa watu wa sampuli iliyotajwa hapo juu kutulia na kuwapa wengine nafasi ya kuwauliza sababu ya matumaini yao, ila husukumia tu watu kinyume cha matakwa yao, nao husahau kabisa upole na hofu". Hao husababisha tu hasara.

Kanuni hii ya Mkombozi na mtume wake lazima ikumbukwe na wote ambao wanao jukumu la kusambaza rekodi na nakala.

Roho ya kiburi au kujimiminia utukufu juu wengine, kwa sababu mtazamo wetu unawiana zaidi na maandiko kuliko yao, daima itawatorosha. Tunaweza kutumia ukweli kama kilabu kuonyesha nguvu yetu kuu tunapo jadili, lakini haita leta watu kwa Mungu. Na kama sheria ya jumla, mpaka tutakapo anza kusikiliza ukweli na kuzingatia kinachosemwa, kuongea tu haita saidia kutimiza mengi.

Tunachotaka ni roho wa upole na upendo wa Kikristo, ambayo, kwa kuwa ni kweli na halisi na wa moyoni, itajidhirisha peke yake kwa yule anayesikiliza na kumwonyesha kuwa nia yetu ni ya kumtenda wema, na wala sio ya manufaa ya kibinafsi na kupata ushindi juu yake. Mtu anaposhawishika kwamba hiyo ndiyo niaya yetu hasa, hiyo itakuwa wa manufaa.

Hatupaswi kuwasukumia watu dini au ukweli kwa nguvu. Hata kama ingewezekana kufanya hivyo, lakini yote hayo bado hayangeweza kutimiza chochote machoni pa Mungu. Anataka kuhudumiwa tu kwa *hiari*. Tukiwa na roho huo wa upendo uliotajwa hapo juu, tutapata mtazamo ule ambao Mwokozi wetu alinenea hapo juu kwenye mada ya somo hili. Kwa maana "hekima itokayo mbinguni kwanza ni safi, kisha ni yenye kupenda amani, mpole na ni rahisis kutumika, iliyo jaa na huruma na matunda mema. Bila vurugu, na bila unafiki". Ni busara itokayo kwingineko tu ndiyo inayofanya watu kutosheka na upendo na ushindi wa kibinafsi, na kuongoza watu kuzingira wenzao bila ya kuwasikiliza. Ni " busaa ya kidunia" inayotokana na ubinafsi.

**—G. I. Butler.**